


## Uchunguzi wa shingo la mfuko wa uzazi ni nini?

Uchunguzi wa shingo la mlango wa uzazi unaweza kugundua mabadiliko katika mlango wa uzazi. Kutibu mabadiliko mapema inaweza kuzuia kansa ya mlango wa uzazi. Uchunguzi wa shingo la mlango wa uzazi ni bila malipo.



## Mlango wa Uzazi ni nini?

Mlango wa uzazi ni mlango uko chini ya uterus. Watoto hutokea mlango wa uzazi wakizaliwa.



## Nini husababisha mabadiliko yasio ya kawaida?

HPV ni virusi vya kibinadamu vya papilloma (Human papillomavirus) inayo ambukizwa kwa tendo la ngono ambayo inaweza sababisha mabadiliko yasio ya kawaida katika mlango wa uzazi wa mwanamke. Mara nyingine mabadiliko yasio ya kawaida husababishwa na HPV inaweza kukua kama kansa. Uchunguzi wa mlango wa uzazi unaweza kugundua mabadiliko isiyo ya kawaida kabla ya kugeuka kuwa kansa.

## Ninahitaji Uchunguzi wa Mlango wa Uzazi?

Wanawake ambao wameshawahi kufanya tendo la ngono (mapenzi na kuguza kimwili) wanastahili kufanya uchunguzi wa shingo la mfuko wa uzazi mara kwa mara.

## Ni mara ngapi ninahitaji kufanya uchunguzi wa uzazi?

Unapaswa kuanza kuwa na vipimo vya Pap kuanzia umri wa 21 na kuendelea baada ya kila miaka 3 hadi umri wa 69.

## Chanjo ya HPV ni gani?

Chanjo ya HPV yaweza kukinga dhidi ya aina fulani za HPV ambazo husababisha kansa ya mlango wa uzazi. Chanjo haitatibu maambukizo ya HPV ambayo iko kwa sasa. Ukipata chanjo, bado unahitaji uchunguzi wa mlango wa uzazi wa kawaida.

## Nitapata Wapi Chanjo?

Uliza mtaalamu wako wa afya, wasiliana na kituo cha afya, au angalia katika interneti kwa [GetCheckedManitoba.ca](http://GetCheckedManitoba.ca).

Kansa nyingi za mlango wa uzazi zinaweza kuzuiwa ikiwa wanawake wanapata uchunguzi wa mlango wa uzazi na kuangaliwa kama kuna mabadiliko yasio ya kawaida.

## Kwa uhusiano zaidi tafadhali wasiliana:

CervixCheck, CancerCare Manitoba  
#5-25 Sherbrook Street  
Winnipeg, Manitoba R3C 2B1

Simu: 204-788-8626  
Bila Malipo: 1-855-952-4325  
[CervixCheck@cancercare.mb.ca](mailto:CervixCheck@cancercare.mb.ca)  
[GetCheckedManitoba.ca](http://GetCheckedManitoba.ca)